# MITAZAMO NA MIENENDO YA UWEZESHAJI WAKULIMA, TANZANIA



SPE
S494
.5.15
M57

- PROGRAMU YA PANTIL
- CHUO KIKUU CHA
- SOKOINE CHA KILIMO

9/2014

# MITAZAMO NA MIENENDO YA UWEZESHAJI WAKULIMA, TANZANIA

FOR REFERENCE
ONLY

PROGRAMU YA PANTIL

CHUO KIKUU CHA

SOKOINE CHA KILIMO

29 MAR 2013

SOKOINE UNIVERSITY OF AGR. LIBRARY
4/8/10

**Kijitabu hiki kimetayarishwa na;**
Dismas L. Mwaseba
Amon Z. Mattee
Zebedayo S. K. Mvena
Everyne A. Lazaro
Raphael M. Wambura
Elimpaa D. Kiranga
Randi Kaarhus

**Kimehaririwa na;**
Emmanuel K. Batamuzi
Dorothy M. Gimbi
Grace E. P. Msoffe
Lusato R. Kurwijila

**ISBN 978 9987 640 57 0**

**Kimechapishwa na:**
Programu ya PANTIL
Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo
Kurugenzi ya Utafiti na Uzamili
S.L. P 3151
CHUO KIKUU, Morogoro, Tanzania
Simu +255 23 2600970; 255 23 3511 na 1102
Faksi +255 23 2600970
Barua pepe: pantilresearch@suanet.ac.tz

**Toleo namba PPN 036**

**© 2010 SUA**



# Dibaji

Kwa miaka kadhaa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kimekuwa kikitekeleza programu nyingi za tafiti zilizokuwa zikifadhiliwa na wahisani mbalimbali. Serikali ya Kifalme ya Norway imekuwa ni mfadhili mkuu aliyekwisha fadhili shughuli za tafiti kadha wa kadha, na tafiti za hivi karibuni ni ile Programu ya Uboreshaji wa Maisha kwa kupitia Mageuzi ya Kilimo na Maliasili (PANTIL). Programu hii ina lengo la kuboresha maisha ya watu wa vijijini kupitia mafunzo, utafiti, na ushauri.

Tofauti na programu za awali ambazo hazikujihusisha moja kwa moja na uwezeshaji wakulima katika mchakato wa kiutekelezaji wake, PANTIL imekifanya kipengele hiki kama moja ya vijipengele vya programu katika muundo wake. Uwezeshaji wakulima unatafsiriwa kama namna ya kuwaongezea wakulima uwezo wa kuwasilisha matakwa yao kuhusiana na maarifa yanayohitajika, tekinolojia na taarifa muafaka ili kuboresha uzalishaji na kupata faida, na hivyo kuchangia katika kuongeza kipato na kupunguza umaskini.

Jopo la watafiti kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) na Chuo Kikuu cha Sayansi za viumbe hai cha Norway (UMB) vilipewa jukumu la kutathmini mitazamo na mienendo ya kuwajengea uwezo wakulima kwa miradi iliyokwishatekelezwa na asasi /miradi na programu mbalimbali katika mikoa iliyoteuliwa ya Tanzania. Ripoti hii ni matokeo ya zoezi hilo. Ripoti inatoa maelezo muhimu juu ya haja ya kujumuisha kipengele cha uwezeshaji wakulima katika tafiti zinazofanywa na SUA pamoja na asasi nyingine hapa nchini na kwingineko. Kwa kupitia ripoti hii msomaji atafaidika katika maeneo yafuatayo: uelewa juu ya dhana ya uwezeshaji wa mkulima, uzoefu wa asasi mbalimbali za kiserikali na zile zisizo za kiserikali kuhusu uwezeshaji mkulima, na mafundisho yatokanayo na shughuli za uwezeshaji.

Prof. J. A. Matovelo

**Mratibu wa PANTIL**

# Shukrani

Tunapenda kuishukuru Serikali ya Kifalme ya Norway kupitia programu ya PANTIL kwa kutupatia fedha zilizotuwezesha kufanya utafiti huu. Tunapenda pia kumshukuru Mratibu wa Programu ya PANTIL, kwa msaada wake kipindi chote cha zoezi hili. Pia tunatoa shukrani kwa msaada tulioupata kutoka kwa watumishi wa asasi/miradi/programu zilizohusika kwenye utafiti. Tunatoa shukrani za dhati kwa wakulima na uongozi wa ngazi ya kijiji kwa kutoa ushirikiano wakati wa utafiti. Pia tunatoa shukrani kwa watafiti na wakurufunzi wenzetu kutoka SUA kwa maoni na michango yao kuhusu kazi hii.



# Yaliyomo

DIBAJI ..... III

SHUKRANI ..... IV

1 UTANGULIZI ..... 1

1.1 MWANZO ..... 1

1.2 HOJA YA KITAFITI/ UMUHIMU WA UTAFITI/TATIZO LILILOPELEKEA UTAFITI KUFANYIKA ..... 2

2. METHODOLOJIA YA UTAFITI ..... 3

3. MATOKEO ..... 5

3.1 TAFITI KUHUSU UWEZESHAJI MKULIMA ..... 5

3.1.1Dhana ya uwezeshaji ..... 6

3.1.2 PANTIL na uwezeshaji ..... 8

3.1.3Vipengele vya uwezeshaji ..... 9

3.2 MTAZAMO WA KIHISTORIA WA UWEZESHAJI TANZANIA ..... 9

3.3 VISABABISHO NA VIKWAZO VYA UWEZESHAJI ..... 11

3.3.1Kusababisha uwezeshaji ..... 11

3.3.2Sababu zinazokwaza uwezeshaji ..... 12

3.4 USHAURI JUU YA MJADALA ZAIDI ..... 14

3.5 KUBUNIWA KWA DHANA YA UWEZESHAJI ..... 14

4. MATOKEO JARABATI ..... 16

4.1 MITAZAMO YA UWEZESHAJI ..... 16

4.2 MATATIZO AMBAYO UWEZESHAJI UNALENGA KUYATATUA ..... 18

4.3 UZOEFU WA HARAKATI ZA UWEZESHAJI MKULIMA ..... 19

4.3.1Utekelezaji wa harakati za uwezeshaji ..... 19

4.3.2Ushirikishwaji katika harakati za uwezeshaji ..... 20

4.4 MITAZAMO KUHUSU SABABU ZINAZOPELEKEA UWEZESHAJI ..... 21

4.4.1Utumiaji wa mbinu shirikishi ..... 21

4.4.2Umadhubuti wa mahusiano baina ya asasi na walengwa ......... 22
4.4.3Mkazo kwenye kujenga uwezo ......... 22
4.5 MBINU ZA UWEZESHAJI ......... 23
5. MAFUNDISHO ......... 27
6. MAPENDEKEZO ......... 28
7. MAREJEO ......... 31
VIAMBATISHO ......... 35



# 1 Utangulizi

## 1.1 Mwanzo

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kimetekeleza tafiti zilizofadhiliwa na Serikali ya Norway kupitia shirika lao la NORAD kuanzia na TAN 90, TAN 20 na TARP - SUA, FOCAL na mwishowe PANTIL. Mradi wa PANTIL una lengo la kuboresha maisha ya watu waishio vijijini kupitia mafunzo kwa vitendo, utafiti, na ushauri. Mradi pia unalenga katika kujenga misingi imara ya utafiti na ushauri kilimo na maliasili inayokidhi mahitaji ya jamii za wakulima na kutoa fursa mpya kwao. Aidha, mradi unatilia mkazo, mbinu fungamanishi ya nyanja anuai na maisha endelevu itakayosaidia walengwa kunufaika na huduma zaidi ya tekinolojia ya kilimo na ufugaji bora.

Kutokana na ripoti ya PANTIL ya mwaka 2005 mradi una vipengele viwili; navyo ni utafiti na uwezeshaji wakulima, na mageuzi ya kitaasisi na kujenga uwezo. Kipengele cha kwanza nacho kimegawanyika katika sehemu vitatu nazo ni (i) tafiti zitokanazo na uhitaji wa tafiti hizo, (ii) uwezeshaji wakulima, na (iii) tafiti ya tathimini ya mfiko/matokeo.

Kipengele cha uwezeshaji mkulima kilibuniwa kwa mtazamo wa kukuza uwezo wa wakulima kuwasilisha matakwa yao juu ya elimu na tekinolojia wanayohitaji ili kuboresha uzalishaji na upataji faida katila kilimo. Pia ilielezwa kwamba, "uwezeshaji unafikiwa pale wakulima watakapojenga uwezo wa kubainisha mahitaji yao na malengo ya uzalishaji, na kuwa na mamlaka, rasilimali na uwezo wa kuwajibisha na kuwa na ushawishi juu ya yaliyomo katika huduma za kilimo za umma na binafsi kama vile ugani, mafunzo, habari, uwekezaji na masoko" (Angalia uk. wa 17).

Aidha, katika nyaraka za mradi wa PANTIL, uwezeshaji wakulima unatekelezwa kupitia shughuli kadhaa zilizoorodheshwa na mradi. Mikakati ifuatayo inapendekezwa:

- Uimarishaji wa vikundi vya wakulima na uanzishwaji wa vikundi vipya kupitia mafunzo juu ya uundaji vikundi, uendeshaji wa vikundi na uongozi;
- Kuwezesha ziara za mafunzo na maonyesho ya kilimo. Shughuli hizi zitahusisha mamlaka za vijiji, na wadau katika huduma za ugani, zikiwemo taasisi zinazotoa mafunzo kwa maafisa ugani;
- Uwezeshaji wa kuanzisha mashamba darasa kwa wakulima katika wilaya na vijiji vilivyoteuliwa;
- Uchapishaji na usambazaji wa elimu, staid na teknolojia kupitia vielelezo, machapisho, vipeperushi, , majarida, vitabu; na
- Uimarishaji wa mbinu za mkulima juu ya mafunzo na uenezaji wa teknolojia mpya kwa wakulima wengine ili kuwafikia walengwa wengi zaidi

Ripoti hii imetokana na utafiti uliolenga kuchangia kwenye kipengele cha utafiti na uwezeshaji wakulima wa mradi wa PANTIL.

## 1.2 Hoja ya kitafiti/ Umuhimu wa utafiti/Tatizo lililopelekea utafiti kufanyika

Zimefanyika jitihada nyingi kuhusu suala la uwezeshaji kwa ujumla na hususan uwezeshaji wakulima hapa Tanzania. Hata hivyo, aina na matokeo ya jitihada hizi hayafahamiki vyema. Hivyo, ili kukamilisha mikakati inayopendekezwa katika kuhamasisha uwezeshaji wa mkulima chini ya PANTIL, ilionekana kuna umuhimu wa kuwa na mjadala wa pamoja na uchambuzi wa kina unaoshughulikia kile kinachofahamika leo kama dhana ya uwezeshaji juu ya masuala na mitazamo ya uwezeshaji. Pia jinsi



elimu ya kijamii, utamaduni na mbinu za michakato ya uwezeshaji inavyo angaliwa na watendaji mbalimbali na kwa mitazamo mbalimbali, na athari zake katika jitihada za maendeleo ya technolojia. Uwezeshaji wa mkulima hauwezi kuchukuliwa kirahisi kuwa ni matokeo ya mikakati ya uwezeshaji tu; hivyo ipo haja ya kutekeleza mikakati hiyo kupitia programu ya PANTIL katika ngazi zote za kinadharia na vitendo.

# 2. Methodolojia ya Utafiti

Hatua ya awali ilihusu mapitio ya maandiko mbalimbali kuhusu tafsiri za maneno na hali ya sasa ya uwezeshaji mkulima katika mazingira ya Kitanzania ili kutoa picha ya jumla na uelewa mzuri wa msingi wa maarifa katika fani hii. Hatua ya pili ilikuwa ni kuyatambua mapungufu ya elimu kuhusiana na uwezeshaji wa mkulima. Tafiti ilichanganua tafiti zilizokwishafanyika mpaka hivi sasa kwa kuzingatia taarifa na mijadala ya kimataifa katika nyanja na mbinu shirikishi kwenye tafiti na uwezeshaji.

Vilevile, taarifa za tafiti zimelenga uzoefu unaoonekana kuhusu njia za kuwezesha hususan uwezeshaji wa mkulima katika mazingira ya Kitanzania. Kwa mfano, kwa miaka mingi zimekuwapo juhudi za uwezeshaji wa aina moja au nyingine ikiwemo mpango wa madaraka mikoani wa mwaka 1970, na utekelezaji wa mageuzi ya serikali za mitaa. Aidha jambo lingine linalofaa kuangaliwa ni utekelezaji wa mkakati wa Serikali kama ulivyoainishwa kwenye Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUKUTA) unaolenga kuwawezesha wakulima wa ngazi ya chini na kuhamasisha uundaji asasi za wakulima kama vyombo vya kuondolea umaskini.

Maandiko husika yanayoelezea uwezeshaji wakulima hapa Tanzania yalipatikana kutoka wizara zenye dhamana ya kilimo, uhakika wa chakula na ushirika, ufugaji, vyuo vikuu, miradi na Asasi zisizo za Kiserikari zilizopo mikoa mbalimbali ya Tanzania. Kwa misingi ya

tafiti, maswali kadhaa ya kitafiti yahusuyo uwezeshaji mkulima na hasa yahusuyo shughuli za uwezeshaji ambayo yanapashwa kujumuishwa kwenye miradi ya PANTIL yaliwekwa bayana. Maswali haya ya kitafiti ndiyo yalikuwa msingi wa tafiti jarabati (empirical study) juu ya uwezeshaji wakulima Tanzania.

Tafiti jarabati ilihusisha ziara za kitafiti kwenye maeneo yaliyoonekana kuwa na uzoefu wenye manufaa kuhusiana na uwezeshaji wakulima, maeneo hayo ni mikoa ya Morogoro, Kilimanjaro, Mbeya, na Dodoma. Ziara zilihusisha jitihada husika za tafiti na programu mbalimbali za kimaendeleo. Wakati wa ziara hizo, taarifa zilikusanywa katika vipengele vitatu. Kipengele cha kwanza kilihusu mahojiano katika ngazi ya taasisi na maafisa wa miradi iliyoteuliwa (Kiambatisho Na. 1). Dodoso lenye maswali ya utambuzi lilitumiwa kama mwongozo kwenye mahojiano na hususan katika kutambua mitazamo mbambali juu ya uwezeshaji wakulima katika maeneo yao. Kipengele cha pili, kilihusu utoaji wa dodoso kwenye sampuli kielelezo ya wakulima kumi katika kila mradi unaojihusisha na mikakati ya uwezeshaji. Dodoso lilikuwa na maswali yaliyokusanya taarifa juu ya vipengele vya uwezeshaji, uzoefu juu ya uwezeshaji na mipaka ya uwezeshaji. Kipengele cha tatu, kililenga majadiliano ya vikundi ambapo kila mradi uliteua wakulima kumi au zaidi kushiriki kwenye mijadala ya vikundi. Mijadala hiyo iliendeshwa kwa kutumia maswali mbalimbali ili kuibua hoja ya masuala kuhusu:

- Mtazamo wa uwezeshaji katika ngazi ya mtendaji;
- Mambo muhimu yanayohitajika katika kuendeleza mradi/shughuli za programu;
- Ripoti ya yale yaliyokwisha fanyika hadi sasa katika kuendeleza mradi/shughuli za programu;
- Matatizo yaliyojitokeza katika kutekeleza shughuli za mradi;
- Urazini wa mradi/jitihada za programu;
- Uzoefu wenye manufaa katika kuendesha na kuendeleza jitihada za mradi; na
- Tathmini ya ndani ya miradi husika.



# 3. Matokeo

## 3.1 Tafiti kuhusu uwezeshaji mkulima

Kwa ujumla, kwenye miaka ya 1970 na 1980 uliwekwa kwenye ushiriki na mbinu shirikishi katika tafiti na maendeleo, uwezeshaji umetokea kuwa miongoni mwa istilahi maarufu ya kimaendeleo kuanzia miaka ya 1990s hadi hii sas. Hamasa za uwezeshaji maendeleo, hususan ile inayohusiana na tafiti na ugani katika kilimo vyaweza kuangaliwa kutokana na kazi ya Scoones na Thompson ya mwaka 1994 *Beyond Farmers First* (Zaidi ya Mkulima Kwanza). Kazi hii ni tahakiki ya kazi ya awali, *Farmer First* (Mkulima kwanza) ya Chambers na wengine ya mwaka 1989 ambazo zimeendeleza mjadala kuhusu maendeleo mbali na ushiriki. Kwa kifupi, *Farmer First* inakazia tafiti na maendeleo yanayozingatia matakwa na shauku ya wakulima. Kama Scoones na Thompson wanavyosema, katika kazi yao ya mwaka 1994, "dhana juu ya *Farmer First* ni kuwa sehemu kubwa ya tatizo la destuli katika utafiti kilimo na ugani liko katika michakato ya kutoa na kuwasilisha tekinolojia, na kwamba mengi ya majibu mengi yatatokana na uwezo na vipaumbele vya wakulima wenyewe. Hata hivyo, ukiangalia dhana ya "*Farmer First",* kikwazo kikubwa cha mtazamo huu upendwao na wengi ni kule kushindwa kwake kuukabili uhusiano ya kimadaraka juu ya mahusiano ya wenyeji na mawakala wa nje wa mabadiliko. Vilevile, mtazamo huu hauoneshi uchanganuzi wa matawi ya kijamii, kiutamaduni na kisiasa yahusuyo ujenzi wa maarifa, ubunifu, utoaji na utumiaji wa teknolojia kwenye jamii za vijijini na asasi za kisayansi" *(*Angalia uk. wa: 2*)*. Jambo hili linasisitizwa pia katika kazi nyingine zilizofuatia kama ile iitwayo Ushiriki: Uonevu Mpya? (*Partcipation: The New Tyranny*?) ya Coooke na Kothari ya mwaka 2001 na Ushiriki: Kutoka uonevu Kuelekea Mageuzi (*Participation: From Tyranny To Transformation*?) ya Hickey na Mohan ya mwaka 2004. Hivyo ni muhimu kwa wakulima na walengwa wengine (mawakala wa mabadiliko wakiwemo watafiti wa kilimo na wafanyakazi wa

ugani), kushughulikia mahusiano ya kimadaraka kama mchakato wa uwezeshaji kwenye tafiti na maendeleo.

Lengo kuu la pitio la maandiko ya ndani na ya kimataifa ni kutoa hoja itakayosaidia kuwa na uelewa mpana zaidi wa uwezeshaji katika ngazi ya nadharia kuhusiana na mitazamo mbalimbali ya dhana ya uwezeshaji. Aidha mapitio hayo yanalenga katika kutafiti na kuhifadhi kimaandishi uzoefu wa kazi za vitendo na wenye mfiko katika mchakato wa uwezeshaji, hususan uwezeshaji wa wakulima, katika mazingira ya Kitanzania.

Pitio hili limegawanyika katika sehemu tatu: Kwanza, ni kuangaliwa kwa dhana ya uwezeshaji kama inavyoonekana kwa watendaji mbalimbali. Pili, ni kujadiliwa kwa vipengele muhimu vya uwezeshaji. Licha ya dhana ya uwezeshaji kuonekana kuwa ni jambo geni, kumekuwa na jitihada kadhaa zilizolenga kuwawezesha watu katika ngazi za kiulimwengu na kitaifa.

Sehemu hii inaelezea kimaandishi baadhi ya tafiti maalum za uwezeshaji nchini Tanzania, ikitilia mkazo juhudi za awali za kipindi cha Ujamaa (Ujamaa wa Kiafrika) na maendeleo katika harakati za ushirika. Kwa kiwango kikubwa juhudi hizi zimekuwa zikifanywa na serikali ikishirikiana na vyama vya kiraia, na hususan Asasi Zisizo za Kiserikali (ASIZE), mashirika ya dini, na vyama vya kijamii, vikiwemo vinavyo jihusisha katika kuhamasisha masuala ya uwezeshaji wa wakulima kwa karibu zaidi. Vilevile kwa hutumia hizi kinachowasilishwa ni mahusiano ya jitihada za uwezeshaji wa mkulima, ikiwemo pia kile kinachoonekana kuwa ni sababu zinazotoa fursa au vikwazokatika uwezeshaji.

### 3.1.1 Dhana ya uwezeshaji

Dhana ya uwezeshaji imeibuka kutokana na fikra kwamba watu kwa ujumla wamekuwa hawana mamlaka, vitu vinavyowafanya wasiwe na ushawishi au uwezo wa kufanya maafikiano ya hali bora na wafanyabiashara, watoa fedha, serikali, na wawakilishi wa vyama



vya kiraia. Wakati huohuo, neno uwezeshaji limekuwa na maana tofauti katika mazingira tofauti ya kijamii, kitamaduni na kisiasa ikiwa na thamani ya kiuhalisia na kinyenzo. Kama ilivyoelezwa kwenye utafiti uliofadhiliwa na DANIDA, "kuzitambua shughuli zinazoweza kupelekea uwezeshaji imekuwa ni suala changamani na kwamba kabrasha la miradi ya uwezeshaji imekuwa na taswira ya anuai kubwa na isiyo na mikakati thabiti.

Katika kazi yake ya mwaka 1999 Cheater analielezea neno uwezeshaji, kama lilivyokuwa likitumika miaka ya 1990 kuwa, linahusu kua msemaji zaidi na kuwa na haki ya kuwa na 'sauti'. Narayan anailezea dhana ya uwezeshaji kama "upanuzi wa raslimali na uwezo wa maskini wa kipato kushiriki, kujadili, kushawishi, kudhibiti, na kuziwajibisha taasisi zinazogusa maisha yao" (Angalia kazi ya Narayan, ya mwaka 2002 uk. wa14).

Vivyo hivyo, wapigania haki za akina mama na wanaharakati wengine wa kijamii (mfano Mosse, 1994) wanatazama uwezeshaji kama ni zaidi ya kupanua wigo wa kufanya maamuzi. Aidha uwezeshaji unapashwa kuhusisha uelewa wa elimumwendo ya uonevu na uonevu uliojengeka. Haya ndiyo yanayo athiri uwezo wa makundi ya wanyonge kushiriki kwenye utoaji maamuzi katika mazingira rasmi au yasiyo rasmi, na kushinikiza ushawishi. Pia namna mtu mmoja mmoja na makundi yanavyoona, na uwezo wao wa kutenda na kuwa na ushawishi katika ulimwengu unaowazunguka. Kwa kuwa uwezo unaohusishwa na kundi fulani la watu, kwa kiasi kikubwa hutokana na jamii, uwezeshaji unapashwa kuhusishwa na kuondokana na miundo hasi ya kijamii, ili kwamba wahusika wajione kuwa wana uwezo na haki ya kutenda na kuwa na ushawishi. Mtazamo huu mpana wa uwezeshaji unaweza kuonekana kuwa na pande tatu, nazo ni mtu binafsi, mahusiano ya karibu, na ya pamoja (Angalia kazi ya Rowlands, 1995). Uwezeshaji, kwa mantiki hii pia unahusisha kubadili mtazamo binafsi na hasa wa yule anayeonewa.

Kulingana na Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi, uwezeshaji unaonekana kama kumuwezesha kila Mtanzania kuwa na jukumu zaidi katika uchumi wa nchi kwa kutengeneza fursa za uwekezaji na mazingira mazuri, ikiwemo kuboresha miundombinu ya kufika kwenye miji mikuu na kutoa upendeleo maalum katika ubinafsishaji wa mashirika ya umma. Kwa mantiki hii, uwezeshaji unaonekana kuwa ni wa mtazamo wa kinyenzo zaidi.

Harakati za ushirika zimekuwa kama eneo mojawapo la uwezeshaji wanachama kiuchumi. Mradi wa MEMCOOP kwa mfano, unaelezea uwezeshaji wa kiuanachama kama juhudi za makusudi za kujenga uwezo miongoni mwa wanachama ili waweze kutoa mwongozo wa mchakato wa ushirika kwa malengo na manufaa yao. Husuan zaidi, kwa muktadha huu, uwezeshaji unatafsiriwa kama "ujenzi na upanuzi wa maarifa, ustadi, utoaji maamuzi, na misingi mingine ya kimadaraka kwa wake na waume, na kwa hiyo kuwajengea uwezo wa kutoa ushawishi na kushika hatamu za uongozi wao wenyewe (Angalia kazi ya Macha, 2003). Uwezeshaji vilevile unatazamwa kama mchakato wa mgawanyo wa madaraka baina ya wanachama wa kawaida na viongozi ili kujenga kujiamini na uwezo wa kuendesha shughuli zao wenyewe. Kwa hiyo, uwezeshaji wa wanachama unaongeza ushiriki zaidi wa wanachama katika ufanyaji maamuzi na ujasiriamali.

### 3.1.2 PANTIL na uwezeshaji

Programu ya PANTIL inauangalia uwezeshaji kama unaojumuisha: uwezo wa wakulima kuwasilisha matakwa yao na malengo, uwezo wa kushawishi maudhui ya huduma za kilimo na kuwafanya watoa huduma wa umma na wale wa sekta binafsi wawajibike zaidi. Hii inamanisha (katika muktadha wa PANTIL), wakulima kuwa na maarifa na taarifa stahiki ili kuweza kubainisha masuala yenye kipaumbele kiutafiti kulingana na mazingira na malengo ya kiuzalishaji. Hii inamaanisha pia kuwa wakulima watahusika kwa karibu zaidi katika upangaji wa shughuli za tafiti, na katika kusimamia rasilimali na matokeo ya tafiti.



Shughuli za uwezeshaji zinazokusudiwa chini ya PANTIL ni kama zifuatazo:

- Mafunzo ili kuimarisha vikundi vya wakulima na kuanzisha makundi mapya;
- Kuandaa ziara za mafunzo, majukwaa ya wakulima, maonesho ya kilimo, ikihusisha wakulima, mamlaka za mitaa, watumishi wa ugani, taasisi za mafunzo, n.k;
- Kusaidia katika uanzishaji wa mashamba darasa;
- Kuwapatia wakulima vifaa vya mafunzo ya ugani, kama vile vipeperushi, vijitabu, nk; na
- Kuwaelimisha wakulima namna ya kusambazaji teknolojia mpya kwa wakulima wengine.

### 3.1.3 Vipengele vya uwezeshaji

Katika kazi yake ya mwaka 2002, Narayan anatambulisha vipengele vikuu vinne vya uwezeshaji, ambavyo kidesturi vinahusika katika miktadha yote. Vipengele hivyo ni upataji wa taarifa, ujumuishwaji na ushrikishwaji, uwajibikaji na uwezo wa kiutendaji wa eneo husika. Kulingana na Narayan, jitihada za uwezeshaji lazima zilenge katika: (a) kuunda taratibu za kusaidia watu kuweza kupata taarifa; (b) taratibu za kusaidia ujumuishwaji na ushrikishwaji; (c) kujenga taratibu za uwajibikaji kijamii; na (d) kuwekeza katika kuwajengea maskini wa kipato uwezo wa kutatua matatizo. Hata hivyo, mtazamo huu hauwezi kushughulikia suala la mahusiano, hili linaweza kuongezwa kama kipengele cha tano cha kujenga ufahamu kuhusu mabadiliko ya kimadaraka sehemu ya kazi katika muktadha wa maisha ya watu, kama inavyoshauriwa na McWhirter katika kazi yake ya mwaka 1991.

## 3.2 Mtazamo wa kihistoria wa uwezeshaji Tanzania

Wakati wa ukoloni, hakukuwa na juhudi za kutosha kuwawezesha watu kiuchumi kwani watu wengi wa vijijini walinyimwa mikopo, elimu, ardhi, na leseni za biashara. Serikali ya kikoloni ilisisitiza

uwezeshaji wa jamii kwa njia ya elimu zaidi badala ya uwezeshaji kiuchumi. Mfano Maghimbi, katika kazi yake ya mwaka 1995 anaeleza kwamba kutoka mwaka 1930 hadi mwaka 1961 (wakati wa uhuru) serikali ya kikoloni ilitoa huduma mbalimbali ikiwemo madarasa ya elimu ya watu wazima.

Hatimae, baada ya Azimio la Arusha la mwaka 1967, watu walihamasishwa kuhamia vijijini ili kuwawezesha kujitegemea na kuleta maendeleo kwa kufuata misingi ya Ujamaa (Angalia kazi ya Nyerere, 1973). Hii inamaanisha kwamba Azimio la Arusha lilikuwa ni jaribio la kuwawezesha Watanzania kumiliki na kuthibiti njia za maendeleo ya kiuchumi katika miundo ya kiitikadi ya kijamaa na kujitegemea. Hapa pia, suala la madaraka halikuwa tatizo kwani madaraka yalikuwa chini ya dola na watu hawakuandaliwa kupingana na dola.

Historia ya uwezeshaji pia inaweza kuangaliwa kama yenye mahusiano ya karibu zaidi na kukua kwa harakati za ushirika Tanzania. Kuzaliwa kwa chama cha wenyeji wapandaji cha Kilimanjaro mwaka 1925 na wakulima waafrika ilikuwa ni matokeo ya taratibu zisizo za haki na ubaguzi wa kisiasa. Kwa hiyo kuanzishwa kwa ushirika wakati huo kulikusudiwa: kuwawezesha wakulima waafrika kupata bei kubwa ya bidhaa zao za kilimo; na kutoa changamoto kwa uongozi wa kichifu na utawala wa kikoloni; na kuhamasisha jamii za kiafrika dhidi ya utawala wa kigeni.

Kwa ujumla, Asasi Zisizo za Kiserikali (AZISE), asasi za dini, na asasi za kijumuiya zimefanya juhudi kuhamasisha uwezeshaji wa mkulima. Kufuatana na asasi hizi uwezeshaji wa mkulima, unamanisha, kuimarisha vyama vya wakulima, kukuza uwezo wa watu masikini wa kipato vijijini wa kusimamia mambo yao wenyewe katika kufanya makubaliano na taasisi za nje na makundi makubwa yenye shauku (Angalia kazi ya DCT, 2004; ya INADES, 1994; MVIWATA). Asasi hizi zimeweka msisitizo kwenye mbinu za utekelezaji wa miradi na shughuli zinazolenga kuimarisha uratibu



baina ya mzalishaji mmoja mmoja, na baadaye miongoni mwa makundi ya kijamii. Mara nyingi, jitihada hizo huongeza mfiko, mahusiano ya mradi na kuwezesha wanachama. Lengo kuu ni kuanzisha asasi za asili endelevu kifedha na kiutawala.

Tathmini iliyofanywa na wataalamu mbalimbali katika asasi/ taasisi mbalimbali imeonesha mahusiano kadhaa baada ya programu/miradi kukamilika. Mahusiano ya michakato ya uwezeshaji iliyojitokeza wakati wa tathmini hii inajumuisha:

- Uboreshaji wa kupata na kudhibiti raslimali binafsi;
- Uwezo wa wakulima/wanavikundi kupata raslimali za umma ikiwemo fursa za elimu, kwa maana wanaweza kushiriki katika programu za mafunzo ndani na nje ya maeneo yao;
- Uboreshaji wa kupata teknolojia mpya na mafunzo ikiwemo kuwapatia wakulima/ vikundi ya wakulima mantiki ya kugawana majukumu na umiliki;
- Uwezo wa wakulima/wanavikundi kupata mikopo ipatikanayo katika maeneo yao na kudhibiti wigo na mchakato wa siasa; na
- Mabadiliko katika nafasi na hadhi katika jamii, hii ni kusema kuwa, mafanikio ya wakulima/vikundi katika kupanua wigo wa kijamii, kufanya mapatano, ujenzi wa mshikamano na kujiamini.

## 3.3 Visababisho na Vikwazo vya Uwezeshaji

### 3.3.1 Kusababisha uwezeshaji

Uwezeshaji unahusisha "uondoaji wa urasimu", na haja ya mtu mmoja mmoja au kwa pamoja, kupata wanachokitaka. Uwezeshaji sio uwakilishi bali unahusu utumiaji wa kiwango cha juu kabisa cha uwezo watu walionao. Ili kulifikia lengo hili, mabadiliko ya kimsingi katika mifumo ya kijamii na kiuchumi na ya kijumuiya yanahitajika katika ngazi mbalimbali. Hii itajumuisha pia haja ya kukuza viwango vya kujiamini na kujielewa miongoni mwa maskini wa kipato na wale wanaonyanyasika kwa namna ambayo itakuza uwezo wao wa kushika hatamu katika maendeleo yao. Hii itahitaji

kukabili matatizo yanayohusiana na viwango vidogo vya kujua kusoma na kuandika, umaskini wa kipato, kutojali, vikwazo vya kiutamaduni na lugha, mbali na mambo mengine.

Vilevile, ili kuwe na uwezeshaji wa watu wasio na fursa nzuri katika jamii panahitajika kuondolewa kwa vikwazo vya kitaasisi zilizo rasmi vinavyochangia washindwe kufanya lolote katika kuboresha maisha yao.

### 3.3.2 Sababu zinazokwaza uwezeshaji

Wakati dhana ya uwezeshaji imekuwa ni wazo muhimu katika msamiati wa maendeleo, kumekuwa na matatizo mengi yanayohusiana na dhana hiyo. Uwezeshaji, mara nyingi umesababisha kuwa na mwamko, ambao umepelekea kuwa na uwezo wa kufikiria mambo kwa makini na hii yaweza kufikiriwa kama suala linaloleta tishio la kisiasa kama ilivyotokea kwa Paulo Freire, Mwaka 1964. Paulo Freire alifungwa jela kwa kuhimiza mageuzi ya kijamii kupitia tafiti za pamoja na baadaye kupelekwa uhamishoni kwa miaka kumi na tano kutoka nchini mwake Brazil (Angalia kazi ya Freedman, 1997). Kulikuwa na hisia kama hizo kipindi cha baada ya uhuru katika mataifa yaliyokuwa makoloni ya Maingereza.

Katika jamii ya sasa, uwezeshaji mara nyingi umekuwa ukilinganishwa na kutotambua mifumo asilia ya kiutawala wa jamii iliyokuwapo. Kwa mfano, uwezeshaji wa akina mama umekuwa mara nyingi ukitafsiriwa kama tishio kwa mfumo dume; wakati uwezeshaji wa wafanyakazi umeonekana kupunguza na kutishia mamlaka za kiutendaji za utawala. Uwezeshaji kama huo katika ngazi za chini unaweza kupelekea maswali kutoka ngazi za chini kuelekezwa ngazi za juu katika mchakato wa maendeleo. Hii inaweza kuonekana kana kwamba ni kutowathamini wataalam wanajiona kuwa ni waangalizi wa maarifa, dhana ambayo kiasili ni mfumo wa mambo kuelekezwa kutoka ngazi ya juu.



Kwa upande mwingine, haja ya kuongeza viwango vya kujiamini na kujithamini miongoni mwa wale wanaonyanyaswa katika namna ambayo itaongeza uwezo wao katika kushika hatamu za kusimamia mambo ni kitu kinachochukua muda mrefu (Angalia kazi ya Rowlands ya mwaka 1995). Ni kwa sababu hii wawezeshaji wa mchakato wa maendeleo huwapendelea wale wenye uwezo wa kushika mambo kwa haraka, wabunifu, kuliko wale 'wazito kuelewa'. Hii inaongeza pengo lililopo kati ya wabunifu na wazito kuelewa.

Kulingana na mitazamo ya maskini wa kipato au kundi la wale wanaonyanyasika katika jamii, uwezeshaji mara nyingi unahusishwa na kuwa na haki zaidi, lakini bila kuwa na wajibu zaidi. Pia uwezeshaji unamaanisha watu kukaa pamoja na kutambua matatizo yao na kuamua mikakati ya pamoja katika kuyashughulikia. Kwa bahati mbaya, watumishi wa asasi za maendeleo, walipowataka watu wa Sudani ya Kusini kufanya kitu kama hiki, waliishia kuwa na orodha ndefu ya mahitaji ya misaada.

Pia kuna utata juu ya tafsiri ya dhana ya uwezeshaji. Mtu anajiona amewezeshwa pale anapopata mgao wa wajibu kimadaraka na utoaji maamuzi, lakini maana ya sasa ya dhana hii haihusishi kuwa na udhibiti wa moja kwa moja wa rasilimali, au wigo wa kujiunga na wengine katika ngazi sawa ya kimfumo ili kuwa na sauti ya pamoja (Angalia African Rights, 1995).

Uwezeshaji pia unakwazwa na mgawanyo wa kimahesabu, unaokwaza utumiaji wa kiwango cha juu cha teknolojia ya habari, kufuatana na sababu kadhaa:

- Viwango vidogo vya elimu, miongoni mwa akina mama vinawatenga akina mama hawa mbali na michakato hii;
- Vikwazo vya lugha, sehemu kubwa ya utaalamu unaweza kuwa katika lugha ambayo jamii maskini haiwezi kuielewa;
- Uwezo duni wa kupata na kumiliki raslimali za kiuchumi;

- Uwezo duni katika kufanya maamuzi;
- Desturi za kitamaduni zinazopitwa na wakati, kwa mfano, ushiriki wa akina mama kwenye duru za kisiasa; na
- Upofu wa jinsia katika mikakati ya maendeleo

## 3.4 Ushauri juu ya mjadala zaidi

Uchambuzi wa hapo juu unaonesha kuwapo kwa masuala kadhaa yanayohitaji kuangaliwa kwa kina, kama vile:

- Kuwapo kwa mitazamo mingi ya dhana ya uwezeshaji. Hata hivyo, kwa ujumla, dhana kuu ya uwezeshaji ni ile ambayo ama mtu anaonekana kuwa na mamlaka /maamuzi au vinginevyo, yaani kutokuwa na madaraka. Kwa mantiki hii uwezeshaji unaweza kuwa kama mchezo wa hesabu za sifuri;
- Kivitendo uwezeshaji unaonekana kuhusisha zaidi uhamishaji wa madaraka kutoka kwa wale wenye madaraka kwenda kwa wale wasio na madaraka. Harakati za uwezeshaji zinazoendelea sasa mfano, mafunzo, na utoaji wa mikopo, unatokana na hii dhana kuu ya uwezeshaji;
- Watendaji wakuu katika michakato ya dhana ya uwezeshaji ni vyombo vya dola na kwa kiasi fulani vyama vya kiraia;
- Kushidwa kwa harakati za uwezeshaji katika nchi kunaweza kukaunganishwa na mwingilio wa dola na unyanyaswaji wa maskini wa kipato au wale waliokusudiwa na harakati hizo; na
- Wakati mfiko wa harakati za uwezeshaji zimewekwa kimaandishi, mifiko itokanayo na michakato hii haifahamiki sana.

## 3.5 Kubuniwa kwa dhana ya uwezeshaji

Kabla ya utafiti, jopo la watafiti lilitafakari dhana ya uwezeshaji kulingana na maandiko yaliyopo. Kwa hali hii, jopo lilibuni vipengele vikuu vya uwezeshaji kuwa ni vile vinavyohusisha yafuatayo:



- Kujiamini;
- Upataji wa maarifa na stadi mpya/raslimali/nyenzo/vitendea kazi
  - Kuboresha maisha, na
  - Kuwa na sauti na mamlaka zaidi katika michakato ya utoaji maamuzi.
- Ushiriki wenye maana.

Viashiria vya vipengele vya uwezeshaji vimewekwa kama ifuatavyo:
- Kujiamini;
- Uwezo wa kuwafanya wengine wawajibike
- Uwezo wa kuhoji mamlaka
- Uwezo wa kufanya mapatano
  - Uwezo wa kushawishi na kubadili tafiti/malengo ya maendeleo
  - Mtazamo wa watu juu ya uwezo wao katika kushawishi mabadiliko ya hapo juu.
- Uwezo wa mfumo/shirika kufikia malengo
  - Uwezo wa kushughulikia/kusimamia migogoro
- Mabadiliko katika maarifa/stadi na tabia
  - Uboreshaji wa upataji taarifa ili kufanya maamuzi ya maana
  - Mahusiano yenye manufaa baina ya watafiti na wakulima (ikihusisha maarifa ya kisayansi/maarifa asilia ya elimumwendo)
- Raslimali/vitendea kazi/umiliki wa nyenzo za kuendeshea maisha
  - Upataji mzuri wa raslimali zinazotosheleza mahitaji.

Sehemu jarabati ya tafiti hii imeongozwa na maswali na malengo kadhaa ya kitafiti (Kiambatisho namba 1)

# 4. Matokeo jarabati

Matokeo yanayoelezwa hapo chini yanatokana na tafiti jarabati ambayo ilihusisha jumla ya programu/miradi saba na asasi moja.

## 4.1 Mitazamo ya uwezeshaji

Asasi nyingi zinazohusika na maendeleo ya vijiji au yale ya kilimo yamekuwa yana uwezeshaji kama ajenda kwenye programu zao. Hata hivyo, asasi hizi zimekuwa zikitilia mkazo vipengele vya uwezeshaji kwa namna mbalimbali tofauti kutegemeana na aina ya msaada wanaotoa kwa jamii husika. Mahojiano na asasi mbalimbali zilizohusika kwenye utafiti huu umeonesha kwamba uwezeshaji kwa walengwa utahusisha moja au zaidi ya mambo yafutayo:

- Kujenga uwezo kwa walengwa kupitia mafunzo ya ufundi, uratibu/uendeshaji, fedha, utawala, na ushawishi, na mbinu za utetezi;
- Kutoa huduma maalum kwa walengwa mfano, mikopo, afya, maji, na elimu;
- Kukuza shughuli za kuleta kipato ili kuongeza kipato cha walengwa;
- Uhamishaji wa moja kwa moja wa rasilimali, ikiwemo utoaji wa misaada ya kifedha, pembejeo, vitendea kazi, vifaa, na mifugo kwa walengwa;
- Kuwahusisha walengwa katika kufanya maamuzi kuhusu usimamiaji na udhibiti wa rasilimali zilizotengwa kwa ajili ya mradi /programu;
- Utoaji wa msaada wa miundombinu kwa walengwa, ikiwemo uboreshaji wa miundombinu ya usafiri na usafirishaji na masoko; na
- Ukuzaji wa uwezo wa kiasasi na kitaasisi kwa mfano utengenezaji na utumiaji wa katiba na uandikishaji rasmi wa vikundi.

Walengwa wa programu/miradi/asasi zilizohusika katika utafiti huu wamekuwa na maoni yanayofanana kuhusu uelewa wao juu ya



uwezeshaji. Kwa maoni yao, uwezeshaji unahusisha moja au zaidi ya mambo yafuatayo:

- Upataji wa maarifa na ujuzi;
- Kupatiwa misaada ya mali;
- Kupatiwa mitaji;
- Kupewa jukumu kubwa zaidi katika kufanya maamuzi juu ya programu; na
- Kufahamu zaidi juu ya shughuli na raslimali fedha za programu/asasi za maendeleo.

Matokeo ya utafiti kwa kutumia dodoso yanaonesha jinsi walengwa wanavyoorodhesha vipengele mbalimbali vya uwezeshaji kwa matabaka (Angalia kiambatisho namba 2). Kufuatana na wahojiwa, wale waliosema uwezeshaji unatazamwa kama machakato wa kupata maarifa mapya walikuwa asilimia 95, wale waliosema ni upataji wa raslimali ni asilimia 88, wale walioona kuwa ni ushiriki katika utoaji maamuzi walikuwa alisimia 39, na wale waliosema kuwa ni kuzifanya asasi za kimaendeleo ziwajibike walikuwa ni asilimia 39. Ongezeko la kiwango cha kujiamini pia ilitajwa na asilimia 39 ya wahojiwa. Matokeo haya yanaonesha kuwa kwa wastani upataji wa maarifa na stadi, na upataji wa fedha na rasilimali nyingine vimekuwa ni njia muhimu ambazo walengwa wanahisi wanaweza kuwezeshwa.

Hata hivyo, jedwali katika kiambatisho linaonesha pia hali ya kutofautiana miongoni mwa taasisi juu ya dhana ya uwezeshaji. Kwa upande mmoja, ni dhahiri kuwa walengwa wanaonufaika na misaada ya INADES walivipa uzito vipengele vya uwezeshaji kulingana na tafsiri iliyotolewa na utafiti huu ikidhihirisha upeo mpana zaidi wa mtazamo kuhusu uwezeshaji. Kwa upande mwingine washiriki katika makundi mengine ya misaada walikuwa na mitazamo finyu zaidi ya dhana ya uwezeshaji. Kwa hakika walengwa wanaonufaika na miradi/programu nne za PADEP, ADP Hombolo na MEMCOOP hawakuona ushiriki, kujiamini na uwezo

wa kufanya mapatano kama vipengele muhimu vya uwezeshaji. Aidha, kwa walengwa hawa, uwezeshaji ulikuwa unaangaliwa kama upatikanaji wa rasilimali, na upataji wa stadi na maarifa mapya. Na kama jedwali linavyoonesha, washiriki wa shughuli zinazosimamiwa na PADEP wanauona uwezeshaji kuwa ni kama unavyoelezewa na vipengele hivi viwili tu.

Mbali ya yote, ni vyema kutambua kuwa uboreshaji/ukuzaji wa upataji wa rasilimali (m.f. ardhi, maji), na kuongezeka kwa uwezo wa kufanya mapatano havikutajwa na asasi yoyote kama ni manufaa ya moja kwa moja ya uwezeshaji. Hii inadhihirisha jinsi dhana ya uwezeshaji inavyotawala, na kuwa iko nje ya kuwa na madaraka.

## 4.2 Matatizo ambayo uwezeshaji unalenga kuyatatua

Taasisi nyingi zimeona kuwa uwezeshaji unalenga kutoa changamoto zifuatazo:

- Mitindo ya maelekezo ya maendeleo kutoka juu badala ya kujenga mitindo ya maelekezo kutoka chini yanayotokana na nguvu ya mahitaji;
- Fikra za muda mfupi kuhusu maendeleo, badala ya kuyaangalia maendeleo kama mchakato wa muda mrefu;
- Mifumo ya masoko ya kiunyonyaji;
- Sera, sheria, tamaduni au taratibu zinazokwamisha maendeleo ya walengwa; na
- Mifumo ya kiutawala ambayo haina maslahi kwa walengwa.

Taasisi zilizohojiwa, yapo maendeleo mengi ya uwezeshaji ambayo yanajumuisha:

- Kuwa na ari ya kujituma na umiliki wa shughuli za maendeleo na matunda yake kwa walengwa wenyewe;
- Kupunguza utegemezi na kuhakikisha kuwa michakato ya maendeleo inakuwa endelevu;



- Kuchochea udhanifu na ubunifu miongoni mwa walengwa mmoja mmoja au kama jamii;
- Kuboresha hali ya kijamii na kiuchumi na kujiamini miongoni mwa walengwa mmoja mmoja au kama jamii;
- Kupunguza upuuzwaji wa walengwa;
- Kuleta utawala bora katika ngazi mbalimbali;
- Kukuza jitihada za maendeleo zitokanazo na nguvu ya mahitaji;
- Kuleta uboreshaji wa maarifa na stadi kwa walengwa mmoja mmoja au jamii.

Dhana yetu ya awali iliangalia uwezeshaji wa wakulima kama unaojumuisha vipengele vifuatavyo:

- Upatikanaji wa maarifa na stadi ;
- Upataji wa raslimali/nyenzo/vitendea kazi katika kuboresha maisha;
- Uwezo wa kuingia makubaliano katika michakato ya utoaji maamuzi;
- Ushiriki wenye maana katika harakati za maendeleo, na
- Kujiamini katika kuwafanya wengine wawajibike na kuhoji mamlaka.

Maoni ya taasisi mbalimbali na walengwa wake yanaelekea kushabihiana na dhana ya uwezeshaji iliyoelezewa na jopo la watafiti. Hata hivyo, ni vyema kuelewa kuwa uboreshaji/kuongezeka kwa upataji rasilimali za asili (ardhi, maji, n.k) na kuongezeka kwa uwezo wa kuingia makubaliano havikutajwa na asasi yoyote kama faida za moja kwa moja za uwezeshaji.

## 4.3 Uzoefu wa harakati za uwezeshaji mkulima

### 4.3.1 Utekelezaji wa harakati za uwezeshaji

Hatua ya kwanza ya uwezeshaji mkulima ni ushirikishwaji katika shughuli zilizopangwa. Kuna namna nyingi ambazo walengwa

wanaweza kushirikishwa kwenye harakati hizo. Uzoefu kutoka kwenye miradi mbalimbali unaonesha kuwa uwezeshaji unaweza kutekelezwa kupitia:

- o Mafunzo
- o Utoaji huduma
- o Ukuzaji wa shughuli zinazoingiza kipato
- o Utoaji wa rasilimali fedha
- o Uimarishaji wa asasi za kiasili.
- o Ushirikishwaji katika shughuli za miradi inayohusu upangaji, usimamiz na tathmini, na
- o Ukuzaji wa mitandao.

### 4.3.2 Ushirikishwaji katika harakati za uwezeshaji

Matokeo ya mahojiano na walengwa wa harakati za uwezeshaji yanaonesha kuwa ushiriki wao katika miradi/asasi ulikuwa na sura mbili. Kwanza walihusika katika miradi kwa kutekeleza jitihada husika. Pili walikuwa na majukumu zaidi ya kutekeleza jitihada hizo. Majukumu hayo, kulingana na mahojiano, yalihusisha kwa mfano, uhamasishaji wa wanakijiji wenzao kushiriki katika miradi. Kwa upande mwingine, wengine walishiriki kama wakufunzi na kama waanzilishi kufuatana na nafasi zao za uongozi.

Kutokana na ufahamu wa malengo ya programu/asasi na mafanikio yake, kwa ujumla, wahojiwa wengi walionyesha kuelewa malengo ya miradi/asasi (Kiambatisho 3). Hii inaonyesha kuwa kuna uhusiano mzuri baina ya walengwa na miradi/asasi, kitu ambacho ni sifa muhimu ya mafanikio katika utekelezaji wa mradi. Kulingana na historia hii, haistajabishi kuona kuwa walengwa wengi (karibia asilimia 70) kama inavyooneshwa kwenye Jedwali (kiambatisho 3) walionesha kuwa miradi/asasi zilifikia malengo yao wakati asilimia 29.2 walisema hayakufikia. Kundi la pili lilitoa sababu kadhaa za miradi/asasi kushidwa kufikia malengo yaliyokusudiwa (Kiambatisho 4). Matokeo ya utafiti yameonesha sababu kuu za miradi/asasi kushindwa kufikia malengo ni upungufu wa rasilimali



za miradi/viwekeza (47.4%) na ukame (36.8%). Katika sababu hizi mbili, upungufu wa rasilimali ulijitokeza mno wakati wa mahojiano na walengwa hususan katika miradi ambayo hutoa rasilimali kwa walengwa kama sehemu ya utekelezaji wa jitihada hizo.

Kama inavyoonesha kwenye jedwali la Kiambatisho 5 wahojiwa kushindwa kwa miradi/asasi kufikia malengo. Karibu wahojiwa wote warioshiriki katika utafiti huu waliliona jambo hili la kushindwa kwa miradi/mashirika. Hii inadhihirisha kwamba mbali na mafanikio yaliyopatikana ya miradi/asasi husika, bado kuna matatizo ambayo huenda yakawa yamerudisha nyuma mafanikio yaliyokwishapatikana.

Jedwali la Kiambatisho 6 linaonesha sababu zinazoathiri utendaji wa miradi/asasi. Ni pamoja na, uhaba wa rasilimali (35.1%), ukosefu wa mafunzo (18.9%) na ukosefu wa masoko ya bidhaa zinazozalishwa (15.5%) Hivi vilitajwa kam vitu vitatu muhimu vinavyoathiri ufanisi wa miradi. Aidha, ni dhahiri kuwa ndani ya miradi/asasi hizi, ukiachia mbali kikundi cha NEEMA (EZCORE) wilaya ya Kilosa, uhaba wa rasilimali ulionekana kuwa ndio sababu kuu inayoathiri ufanisi.

## 4.4 Mitazamo kuhusu sababu zinazopelekea uwezeshaji

Sambamba na mitazamo kuhusu mambo yanayosababisha uwezeshaji, asasi na walengwa mbalimbali walikuwa na maoni yafuatayo kuhusu sababu za uwezeshaji:

### 4.4.1 Utumiaji wa mbinu shirikishi

Asasi zinachukulia matumizi ya mbinu shirikishi hususan Ukuzaji wa Mbinu Shirikishi ya Utafiti (*Participatory Rural Appraisal* - PRA) kama njia ya uhakika ya uwezeshaji wa walengwa. Kwa uhalisia wake, mbinu shirikishi zinatoa fursa kwa walengwa kushiriki katika utoaji wa maamuzi ya nini kifanyike na kwa namna



SOKOINE UNIVERSITY OF AG

gani, na kujenga kujiamini na stadi kwa walengwa kushika hatamu za mchakato wa maendeleo yao wenyewe. Lengo mahususi la mbinu ya PRA ni kuupa chachu mchakato unaopelekea kwenye mifumo mipya ya uelewa na kujiamini wenyewe. Hakika, PRA imetoa fursa nzuri ya kuvumbua namna ambavyo uzoefu, na matakwa na mitazamo tofauti ya makundi lengwa yanavyotofautiana (Angalia kazi ya Mosse, 1994).

Kufuatana na maoni ya walengwa, mbinu shirikishi inaimarisha stadi zao za kufanya maamuzi, inaongeza uwezo wa kufanya mapatano na wageni na, kwa ujumla, inaboresha stadi zao katika jitihada za kufanya mipango ya maendeleo.

### 4.4.2 Umadhubuti wa mahusiano baina ya asasi na walengwa

Uwezeshaji una nafasi kubwa pale palipo na ushirikiano wa muda mrefu baina ya asasi na walengwa wake; na ambapo mahusiano hayo yamejengwa katika misingi ya usawa, ushirikiano na kuheshimiana. Ili kuwa na mfiko, asasi zilionelea ni vyema kukawa na uhusiano na walengwa katika mifumo ya ushirikiano wa muda mrefu, unahohakikisha umadhubuti, uelewekaji na uendelevu. Hii itajenga maelewano, kuaminiana na hatimaye kuleta matokeo yanayoonekana ikiwemo uboreshaji wa maisha na uimarishaji wa asasi za asili. Hii inategemea misingi madhubuti ya raslimali, ikiwemo fedha, watu na mali. Walengwa pia wataona kuwa kuendelea kwa mahusiano na asasi za maendeleo ni jambo muhimu katika kuleta matokeo yanayoonekana na uwezeshaji. Kufuatana na maoni yao, kuendeleza mahusianao kunapunguza kiwango cha kushindwa kwa miradi.

### 4.4.3 Mkazo kwenye kujenga uwezo

Sambamba na maoni ya wengi kuwa uwezeshaji ni upataji rasilimali na maarifa mapya, asasi pamoja na walengwa wao pia wanachukulia



kujenga uwezo kiufundi, kifedha na kiasasi kama kigezo muhimu cha uwezeshaji. Hakika, vipengele hivyo vitatu lazima vizingatiwe katika uwiano sahihi ili jitihada ziweze kuzaa matunda na kuleta mabadiliko endelevu.

Katika kutupia jicho kujenga uwezo, maarifa na stadi, tabia na uwezo wa walengwa vinaweza kuimarishwa; na hii huongeza fursa ya mafanikio ya jitihada za miradi na hatimaye kujenga uwezo wa walengwa kujiamini na kushiriki katika jitihada za maendeleo kwa siku za usoni.

## 4.5 Mbinu za uwezeshaji

Miradi na asasi zote zilizopitiwa zilijihusisha katika moja au zaidi ya mambo yafuatayo: mafunzo, utoaji huduma, ukuzaji wa shughuli za kujiongezea kipato, utoaji wa rasilimali fedha, uimarishaji wa asasi za asili, ushiriki katika shughuli za miradi, upangaji mipango, usimamizi, na tathmini; na ukuzaji wa mitandao. Hata hivyo, asasi hizi zilionekana kana kwamba zinatumia mbinu tofauti kidogo katika harakati zao za uwezeshaji kutegemeana na maeneo yao ya kipaumbele kama inavyoonekana kwenye muhtasri ufuatao.

INADES: asasi hii inaweka mkazo mkubwa katika maendeleo ya kitaasisi ya kundi lengwa kupitia mafunzo ya mbinu za uongozi, uundaji na uendeshaji vikundi. Juhudi kubwa zinawekwa katika kuwezesha makundi lengwa kujijengea uwezo katika kujisimamia wenyewe na kushirikiana na wengine. Kwa upande mwingine INADES, haitoi msaada wowote wa moja kwa moja wa mali au fedha kwa makundi lengwa mbali na mafunzo, ufuatiliaji, na kuwaunganisha na watoa huduma wengine.

Wakati huo huo, mbinu ya kujifunza kwa vitendo pia inategemewa kuwa na uwezeshaji kwani inaruhusu makundi lengwa kushiriki kikamilifu katika kutambua mahitaji yao ya kimafunzo na inatoa

fursa kwa makundi lengwa kuwa na tathmini ya kina juu ya hali zao, na hatimaye kuweza kuchukua hatua madhubuti kuboresha hali hizo.

Mfumo huu umewezesha kuwa na ongezeko kubwa la ari ya kujiamini na kujitegemea miongoni mwa wanavikundi lengwa. Ari ya kujitegemea imewawezesha wanavikundi kuchagua viongozi bora miongoni mwao wenyewe na kuweza kuwashinikiza zaidi katika suala la uwajibikaji, mbali na uboreshaji stadi, katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za kuongeza kipato.

Asasi DCT imeweka mkazo zaidi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo, kwa kiwango kikubwa, imejumuisha msaada wa mali kwa kikundi lengwa ikiwemo pia stadi za ufundi zinazohusiana na maeneo yanayoshughulikiwa na mradi. Aidha, sambamba na jukumu lake kama asasi ya kidini, DCT imejihusisha zaidi katika utoaji huduma za jamii (maji, afya, elimu) katika makundi yake mbalimbali, na iko katika mstari wa mbele katika utoaji huduma za dharura itokeapo majanga kwa mfan, ukame au mafuriko. Ni katika siku za karibuni tu ndipo ilipoanza kujihusisha na maendeleo ya kitaasisi kwa makundi lengwa (kupitia mafunzo katika uundaji vikundi).

Mbinu zinazotumiwa na DCT zimepelekea kuwapo na ongezeko la fursa za shughuli za kujiongezea kipato miongoni mwa makundi lengwa, lakini pia wakati huo huo imedumisha hali ya utegemezi, ambapo watu wanakosa kujiamini vya kutosha katika utendaji wao bila kutegemea msaada kutoka DCT.

MEMCOOP: Mradi huu ulio chini ya Chuo cha Ushirika Moshi, umehusisha mafunzo kwa wanaushirika ili waweze kubeba majukumu muhimu zaidi katika vyama vyao vya ushirika. Mafunzo yalikusudia kuwapa stadi na uwezo wa kujiamini kuongoza, na kushinikiza uwajibikaji wa viongozi wao na kuchangia kama wanachama wa kawaida katika maendeleo ya vyama vyao vya ushirika kwa ujumla. Kwa hiyo, mafunzo yalilenga kwenye misingi



ya ushirika, lakini muhimu zaidi, ni juu ya stadi binafsi za wakurufunzi. Mbinu ya mafunzo ilikuwa shirikishi kwa maana kwamba iliruhusu mijadala mikali juu ya mada mbalimbali miongoni mwa wakurufunzi.

Mradi wa MEMCOOP umepelekea kuwa na maboresho makubwa juu ya uongozi na utendaji wa vyama vya ushirika kwa ujumla katika maeneo ya mradi kwa kuwa wanaushirika wameboresha stadi zao za uongozi na ujasiliamali, na hata uwezo wa kujiamini.

Mradi wa PADEP: ni mradi wa serikali unaotekelezwa kupitia serikali za mitaa katika wilaya teule. Mradi unalenga kuwezesha makundi lengwa kupitia mafunzo ya stadi shirikishi na ufundi, na kupitia utoaji fursa katika kutambua na kusimamia miradi yao ya maendeleo kwa rasilimali fedha zitolewazo na mradi.

Tofauti na mbinu za kidesturi za mradi, ambapo miradi husanifiwa katika ngazi za juu, katika PADEP makundi lengwa ndiyo yanayohusika katika kutambua miradi ya kufaa, kuingia mikataba na watoa huduma mbalimbali (wa umma na binafsi), na katika usimamiaji wa utekelezaji wa miradi.

Mbali na utoaji rasilimali fedha moja kwa moja, na kuruhusu makundi lengwa kuamua juu ya jitihada zinazotakiwa, PADEP imejenga uwezo wa makundi lengwa kupanga na kutekeleza miradi ya maendeleo, kufanya mapatano ya kibiashara na kushughulikia mikataba baina yao na watoa huduma mbalimbali, na imewaongezea uwezo wa kujiamini katika ufanyaji shughuli na watendaji wengine ikiwemo watumishi wa Wilaya, taasisi za fedha, asasi za kibiashara, na AZISE.

Mradi wa EZCORE umelenga katika kuwezesha kundi lengwa kuwa na mchango katika kufanya maamuzi kuhusu ajenda za tafiti katika utafiti wa kilimo. Lengo hili limefikiwa kupitia uundaji wa jukwaa la ushauri ikishirikisha watafiti, wawakilishi wa wakulima na

Halmashauri za Wilaya, ambapo masuala ya kipaumbele kuhusu tafiti yaliafikiwa. Vilevile, baadhi ya shughuli za tafiti zinahusisha makundi ya utafiti ya wakulima yanayoshirikiana na watafiti katika utekelezaji wa majaribio ya tafiti kwa namna shirikishi. Wakulima wanaohusika katika majaribio mbalimbali ya tafiti walipewa mafunzo katika stadi mbalimbali za ufundi na walihusika pia katika ziara za mafunzo ili kujenga uwezo wa kujiamini.

Mradi wa EZCORE umetoa fursa kwa makundi lengwa kuwa na sauti katika masuala yanayohitaji huduma za watafiti, hata hivyo mfiko muhimu zaidi ni uwezo wa halmashauri za wilaya kuingia mikataba na watafiti katika kuhakikisha kuwa shughuli za tafiti zinaendeshwa kwa manufaa ya wilaya husika.

Mradi wa MSDPunaendeshwa na serikali. Mradi huu unaolenga katika kuboresha upatikanaji wa soko kwa wakulima; unajaribu kufikia lengo hilo kwa kutoa mafunzo na miundombinu mbalimbali ihusuyo mambo ya soko. Japokuwa kundi lengwa la msingi ni wakulima, mradi pia umehusisha asasi zingine kama vile halmashauri za wilaya, TCCIA, ushirika wa masoko, na AZISE na asasi nyingine za kijamii zilizohusika kwa njia moja au nyingine katika utafutaji soko la mazao ya walengwa. Utoaji mafunzo kwa wanavikundi umehusisha zaidi mafunzo kwa watoa huduma walioteuliwa na mradi.

Mradi umefanikisha kuwa na upatikanaji wa soko kama matokeo ya uboreshaji wa miundombinu. Na vile vile mradi umefanikisha kuongeza uwezo wa kujiamini miongoni mwa wazalishaji katika kufanya mapatano ya hali bora zaidi ya kibishara kwa bidhaa zao.

Programu ya RFSP inakusudia kuboresha upatikanaji wa huduma za kifedha kwa wakulima, kupitia uimarishaji wa usimamizi wa taasisi ndogo ndogo za kifedha (MFIs). Mradi umejikita katika utoaji mafunzo kwa wanachama na viongozi wa taasisi hizi ndogo ndogo za kifedha ili kuziongezea uwezo kiutendaji. Msaada ulihusu



mafunzo ya majumbani na yale ya sehemu za kazi, ufuatiliaji wa karibu na utelekezaji, na ziara za mafunzo miongoni mwa wanachama ili kubadilishana mawazo, kujenga mitandao na kujenga uwezo wa kujiamini.

Mpango huu umechangia kwa kiasi kikubwa uboreshaji wa utendaji wa taasisi ndogo ndogo za kifedha (MFIs) katika eneo la mradi. Hii inatokana na ukweli kuwa mradi umeboresha stadi na hivyo kujiamini kwa viongozi na watumishi juu ya namna ya kuendesha taasisi hizi.

Chama cha Msingi cha Ushirika cha Mkuyuni (Mkuyuni Primary Cooperative Society). Hiki ni chama cha msingi cha ushirika wa masoko ya kilimo kinachokusudia kuwawezesha wanachama kupata bei nzuri ya mazao yao. Chama kimeshafanya shughuli mbalimbali ikiwemo kutoa mafunzo kwa wanachama juu ya misingi ya ushirika, kukuza tabia ya kuweka akiba miongoni mwa wanachama, na kuanzisha mfuko wa ununuzi mazao ili kuruhusu mazao kununuliwa kutoka kwa wanachama hata kama hakuna mkopo wa benki.

Chama cha ushirika kimefanikiwa kufikia lengo lake la kuwa wakala wa ununuzi wa mazao kutoka kwa wanachama na kutawanya pembejeo miongoni mwa wanachama. Kwa kiasi kikubwa chama kimekuwa kikiendeshwa kufuatana na katiba na misingi ya ushirika.

## 5. Mafundisho

Kutokana na matokeo ya tafiti, ni dhahiri kwamba zifuatazo ni sababu muhimu zinazoweza kuliwezesha kundi lolote lile.

i. Kujenga uwezo kupitia mafunzo juu ya maarifa na stadi za kitaasisi na kiufundi, kwa vile kigezo hiki kinajenga uwezo wa kujiamini kwa makundi lengwa katika kuchukua hatua zaidi kuelekea 'uwezeshaji'.

ii. Kutambua kuwa maarifa na stadi bila raslimali vinaweza visilete matokeo yoyote kwa makundi lengwa, hivyo ni muhimu kuwa mafunzo yaendane na utoaji wa raslimali ama yajumuishe maarifa na stadi za kujiletea kipato, au taarifa juu ya sehemu zinapopatikan rasilimali.

iii. Kwa maana ile ile, utoaji wa rasilimali pekee bila ya kujenga uwezo wa kutosha kwa vikundi lengwa hakutaleta mabadiliko endelevu, bali kutasababisha kuendeleza utegemezi na si uwezeshaji.

iv. Ili kushughulikia suala la mfumo wa utawala na kuongeza uwezo wa vikundi lengwa wa kuamua na kutenda, kama vile, kuwaongezea nguvu za kisiasa, ni muhimu kuanza harakati za kuuvunja upweke na kujenga mshikamano. Kwa hiyo harakati za uwezeshaji ni budi zihusishe ujenzi wa asasi za msingi zenye nguvu, na ni budi zijenge mitandao na ushirikiano miongoni mwa asasi ili kuweza kusikika na kuonekana zaidi.

v. Kufikia uwezeshaji wa kweli ingawa kunahitaji muda na mahusiano endelevu baina ya taasisi na makundi lengwa. Maelewano ya pamoja na kuaminiana ni budi vijengwe baina ya taasisi na makundi lengwa, na hili linachukua muda mrefu na mawasiliano ya karibu ya mara kwa mara.

vi. Kujenga mazingira ya kisiasa yanayohamasisha na kukuza uwezeshaji, vinginevyo mfiko wa harakati za uwezeshaji zitaishia kwenye maeneo machache na hatimaye hayatakuwa endelevu kwa vile mazingira ya kisiasa yanaweza kupunguza kwa haraka makali ya mfiko.

# 6. Mapendekezo

Mapendekezo yafuatayo yametolewa kwa kuzingatia mipango na mikakati ya mradi wa PANTIL

a) Kuhusu kipengele cha uwezeshaji cha mradi wa PANTIL: mbali na kile kilichopendekezwa ndani ya mradi wa PANTIL, hatua zifuatazo zinapendekezwa:



i. Kutambua makundi lengwa maalum (m.f. makundi ya uzalishaji, makundi ya tafiti, vyama vya ushirika n.k) ambavyo yataweza kufanya nao kazi katika misingi endelevu, na hapana budi shughuli zote za uwezeshaji zielekezwe kwenye makundi haya.

ii. Kutambua taasisi, miradi n.k. ziendeshazo shughuli zake katika maeneo husika au na vikundi vilivyoteuliwa na kuanzisha mahusiano navyo ili kuweka juhudi za pamoja. Aidha, ni vyema halmashauri za wilaya zikawa zinataarifiwa juu ya kile kinachoendelea katika maeneo yao.

iii. Kutumia mbinu shirikishi katika kupata mahitaji ya kimafunzo ya makundi hayo kuhusiana na uwezeshaji, na kwa pamoja kutengeneza viashiria vya uwezeshaji.

iv. Kuanzisha kwa pamoja makundi lengwa mifumo ya kitaasisi/kamati za kutathmini maendeleo na mfiko wa shughuli za PANTIL katika ngazi za chini.

v. Kutilia mkazo uboreshaji wa vipato vya makundi lengwa kama moja ya vivutio muhimu kwa ushiriki wao na mahusiano.

b) Kwa upande wa kipengele cha tafiti cha PANTIL, inashauriwa kwamba watafiti hawana budi:

i. Kuunda jukwaa la ushauri kwa kila mradi wa utafiti, ikihusisha watafiti, wakulima na wadau wengine muhimu, ambapo maendeleo ya tafiti na matokeo yake yatakuwa yanaendelea kutathminiwa mfululizo.

ii. Wawe na uwezo wa kubadilika kufuatana na hali halisi katika michakato yao ya tafiti, wakitilia maanani ushauri kutoka kwa makundi lengwa, na uzoefu uliopatikana kwenye uwanja wa tafiti, ili kuweza hatimaye kupata matokeo ya tafiti yanayoweza kuwa na manufaa ya moja kwa moja kwa makundi lengwa.

iii. Kuzingatia uendelevu wa shughuli na matokeo ya mradi hata baada ya PANTIL kufikia ukomo, kwa kufanya kazi na makundi lengwa ili kujenga mikakati sahihi iliyopo.



# 7. Marejeo


African Rights (1995), Imposing empowerment? Aid and civil institutions in Southern Sudan. Discussion Paper No. 7 (December) London: African Rights.

Batliwala, S. (1993), Empowerment of women in South Asia: concepts and practice New Delbhi: Asia-South Pacific Bureau of Adult Education and Freedom from Hunger Campaign.

Bebbington, A.J., D. Merril-Sands and A.J. Farrington (No date), Farmer and community organizations in agricultural research and extension: functions, impacts and questions. IRDC Currents No. 11.

Chambers, R., A. Pacey and L.A. Thrupp (eds.) (1989), Farmer first: farmer innovation and agricultural research. Intermediate Books Publications: London

Cheater, A. (ed.) (1999). The anthropology of power: empowerment and disempowerment in changing structures. Routledge: London and New York.

Cooke, B. and U. Kothari (2001), Participation: The new tyranny? ZED Books: London and New York.

DCT (2004), Diocese of Central Taganyika: Evaluation of Itiso household food security programume for the people from July to June 2004. A Final Report July 2004, Development Services Company Ltd, Tanzania.

Freedman, J. (1997). Accountability in the participatory mode. Canadian Journal of Development Studies XVIII, Special Issue.

Hickey, S. and G Mohan (eds.) (2004). Participation: From taranny to transformation? ZED Books: London and New York.

INADES Fornation Tanzania (1999). Orientations and plan of action: in support of farmer organizations 1999-2001. INADES Formation Tanzania, Dodoma.

Macha, F. A. (2003). Member empowerment in co-operatives: Project experiences in Kilimanjaro region. Journal of Co-operative and Business Studies, Vo. 1:1-29.

Maghimbi, S. (1995). The conflict between the state and grassroots-based institutions in Tanzania's rural development. In: C. Foster and S. Maghimbi (eds.). The Tanzania peasantry: Further Studies. Aldershort: Avebury.

McWhirter, E.H. (1991. Empowerment in counseling. Journal of Counselling and Developmernt 69 (3): 222-27.

Ministry of Cooperatives and Marketing (2005). Cooperative reform and mordernisation programme (CRMP) (2004/2007).

Mosse, D. (1994), Authority, gender and knowledge: Theoretical reflections on the practice of participatory rural appraisal. Development and Change, Vol. 25. 497-526.

MVIWATA (2004) National Network of Farmers' Organisations in Tanzania: The strategic plan 2004-2008, Morogoro, Tanzania.



Narayan, D. (ed.) (2002) Empowerment and poverty reduction a soucfre book. World Bank: Washington D.C.

Nyerere, J.K. (1967). Education for self-relience. Government printer: Dar es Salaam.

Nyerere, J.K. (1973). Freedom and development. Oxford Universsiy Press: Dar es Salaam.

PANTIL (2005). Programme for agricultural and natural resources transformation for improved livelihoods. Programme Document for the Period July 2005 to June 2009. Sokoine University of Agriculture. Morogoro, Tanzania.

Parpart, J.L. (2000). The Participatory empowerment approach to gender and development in Africa: panacea or illusion? Occasional Paper, Centre of African Studies: University of Copenhagen.

Rowlands, J. (1995). Empowerment examined. Development in Practice, Vol. 5 (2): 101-107.

Scones, I. and J. Thompson (eds.) (1994), Beyond farmer first: rural people's knowledge, agricultural research and extension practice. Intermediate Technology Publications: London.

Technical Advisory Service (2004). Farmer empowerment experiences, lessons learned and ways foward. Vol. 1: Technical Paper: DANIDA, December 2004. United Republic of Tanzania (1969), Presidential Circular No. 1 of 1969. Government Printers, Dar es Salaam.

United Republic of Tanzania (1998). Farmer empowerment and organization in Tanzania. Current situation and recommendations for strategic interventions. Final Report. Dar es Salaam, ASDP Secretariat, Ministry of Agriculture and Food Security.

United Republic of Tanzania (2004a). National Strategy for Growth and Reduction of Poverty (NSGRP) (MKUKUTA). Government Printer, Dar es Salaam.

United Republic of Tanzania (2004b). The national economic empowerment policy. The Prime Minister's Office



# Viambatisho

**Kiambatisho 1: Malengo na maswali ya dodoso**

| | Lengo | Swali la kitafiti |
|---|---|---|
| 1 | Kuchunguza mitazamo ya uwezeshaji mkulima ya watendaji muhimu katika tafiti na maendeleo | o Ni kwa vipi uwezeshaji mkulima unaangaliwa na watendaji muhimu katika ngazi ya taasisi na mtendaji?.<br>o Uwezeshaji una kusudia kutatua matatizo gani?<br>o Ni kwa kiwango gani mtazamo wa watendaji muhimu kuhusu uwezeshaji unashabihiana na tafsiri ya uwezeshaji iliyotolewa katika tafiti inayopendekezwa? |
| 2 | Kuchanganua uzoefu wa jitihada mbalimbali za uwezeshaji mkulima nchini | o Ni sababu zipi zinachangia mafanikio au kushindwa kwa juhudi za uwezeshaji mkulima kama zinavyotafsiriwa na watendaji muhimu?<br>o Ni kwa vipi watendaji mbalimbali wanaelezea na kutathimini uzoefu wao katika jitihada za uwezeshaji?<br>o Ni kwa vipi uwezeshaji mkulima unatekelezwa?<br>o Ni kwa kiwango gani jitihada za uwezeshaji mkulima zenye mafanikio zinajumuisha vipengele / viashiria vya uwezeshaji kama vinavyotafsiriwa kwenye tafiti? |

| | | |
|---|---|---|
| 3 | Kupendekeza mikakati ya uwezeshaji mkulima ndani ya muundo wa PANTIL | o Ni kwa vipi PANTIL na miradi yake imepangwa kufanikisha uwezeshaji mkulima?<br>o Kulingana na yaliyotajwa hapo juu, ni kwa vipi watafiti wa PANTIL wamejumuisha / wametekeleza / wameendesha shughuli kwa vitendo zitakazopelekea uwezeshaji mkulima? |



**Kiambatisho 2: Mtazamo wa wahojiwa juu ya uwezeshaji (N=77)**

| Jina la Asasi | Mtazamo wa wahojiwa juu ya uwezeshaji | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Ushiriki | Kujiamini | Upataji rasilimali | Uwezo wa kujadiliana | Upataji wa maarifa mapya |
| AMSDP | 5 | 5 | 9 | 5 | 9 |
| RFSP | 4 | 8 | 9 | 5 | 9 |
| INADES | 6 | 7 | 7 | 7 | 9 |
| DCT | 2 | 1 | 7 | 0 | 7 |
| Mkuyuni Cooperative Society | 6 | 5 | 9 | 49 | 10 |
| EZCORE | 6 | 3 | 10 | 6 | 10 |
| PADEP | 0 | 0 | 10 | 0 | 10 |
| MEMCOOP | 1 | 1 | 6 | 3 | 9 |
| Jumla | 30 (39) | 30 (39) | 67 (88) | 30 (39) | 73 (95) |

*Takwimu kwenye mabano zinaonyesha asilimia*

**Kiambatisho 3: Ufahamu wa ufikiaji malengo ya mradi**

| Ufahamu wa ufikiaji malengo ya mradi | | |
|---|---|---|
| Jibu | Idadi ya marudio | Asilimia |
| Ndiyo | 73 | 94.8 |
| Hapana | 4 | 5.2 |
| Jumla | 77 | 100 |
| Mafanikio ya malengo ya miradi/asasi | | |
| Ndiyo | 51 | 70.8 |
| Hapana | 21 | 29.2 |
| Jumla | 72 | 100 |

### Kiambatisho 4: sababu za miradi/asasi kushindwa kufikia malengo (n=19)

| Mradi/Asasi | Sababu zilizotajwa na makundi lengwa | | | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kufikia malengo ya mradi | Uhaba wa rasilimali za mradi/ viwekeza | Uongozi mbovu | Katiba mbovu | Ukame | |
| AMSDP | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 2 |
| RFSP | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| INADES | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| DCT | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| Mkuyuni Co. Society | 0 | 5 | 1 | 1 | 1 | 8 |
| EZCORE | 0 | 1 | 0 | 0 | 2 | 2 |
| PADEP | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 2 |
| MEMCOOP | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 2 |
| Jumla | 1(5) | 9(47.4) | 1(5) | 1(5) | 7(36.8) | 19(100) |

### Kiambatisho 5: Matokeo ya kushindwa kwa miradi/asasi

| | Jibu | | Jumla |
|---|---|---|---|
| Mradi/ Asasi | Ndiyo | Hapana | |
| AMSDP | 9 | 1 | 10 |
| RFSP | 6 | 3 | 9 |
| INADES | 8 | 1 | 9 |
| DCT | 8 | 2 | 10 |
| Mkuyuni Cooperative Society | 10 | 0 | 10 |
| EZCORE | 9 | 0 | 9 |
| PADEP | 8 | 2 | 10 |
| MEMCOOP | 7 | 1 | 8 |
| Jumla | 65 | 10 | 75 |



### Kiambatisho 6: Sababu zinazoathiri ufanisi

| Mradi/Asasi | Kufikia malengo ya mradi | Uhaba wa rasilimali za mradi | Ukosefu wa masoko ya bidhaa | Miuondombinu mibovu | Uhaba wa mvua | Ukosefu wa msimamo imara kwa wanachama |
|---|---|---|---|---|---|---|
| AMSDP | 4 (18.2) | 10 (45.5) | 4 (18.2) | 4 (18.2) | 0 (0.0) | 0 (0.0) |
| RFSP | 5 (22.7) | 8 (36.4) | 5 (22.7) | 3 (13.6) | 0 (0.0) | 1 (4.5) |
| INADES | 2 (15.4) | 6 (46.2) | 0 (0.0) | 1 (7.7) | 0 (0.0) | 3 (4.5) |
| DCT | 1 (6.3) | 7 (43.8) | 0 (0.0) | 0 (0.0) | 6 (37.5) | 2 (12.5) |
| Mkuyuni Cooperative Society | 5 (22.7) | 7 (31.8) | 5 (22.7) | 0 (0.0) | 0 (0.0) | 5 (22.7) |
| EZCORE | 8 (33.3) | 5 (20.8) | 5 (20.8) | 4 (16.7) | 1 (4.2) | 1 (4.2) |
| PADEP | 1 (7.1) | 4 (28.6) | 2 (14.3) | 0 (0.0) | 3 (21.4) | 4 (28.6) |
| MEMCOOP | 2 (13.3) | 5 (33.3) | 2 (13.3) | 0 (0.0) | 4 (26.7) | 2 (13.3) |
| Jumla | 28 (18.9) | 52 (35.1) | 23 (15.5) | 12(8.1) | 14 (9.5) | 18 (12.2) |

### Kiambatisho cha 7: Asasi zilizofanyiwa utafiti

| Taasisi | Mahali |
|---|---|
| DCT | Dodoma Vijijini/Dodoma |
| INADES | Kongwa/Dodoma |
| PADEP | Hai/Kilimanjaro |
| EZCORE | Kilosa/Morogoro |
| MEMCOOP | Hai/Kilimanjaro |
| Mkuyuni Primary Coop | Morogoro |
| AMSDP | Mbeya |
| RFSP | Mbeya |

SPE
S494
.5.I5
M57
copy 3

ISBN 978 9987 640 57 0

Printed by Inter Press of Tanzania Ltd.